## MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA

**Karatasi ya Maswali: namba 11.**

Jaribu kuyajibu maswali yafuatayo kwa maneno yako mwenyewe. Pale palipoandikwa ‘Kazi ya ziada’, unaweza kulijibu swali kama unapenda, au kuliacha kama unaona ni gumu mno. Tafadhali jaribu kuyajibu maswali mengine yote.

**Masomo: 41-44**

37. (a) Tunaweza kujifunza nini kutokana na jinsi Adamu na Hawa walivyowalea watoto wao?
    (b) Ibrahimu anatupa kielelezo gani kuhusiana na maisha katika familia?
    (c) Paulo hukuwa baba yake Timotheo, lakini ni vipi anavyomchukulia? Hili linatufundisha nini?
    (d) Mzazi anaweza kumwasha-kibao mtoto?

    Kazi ya ziada.
    (e) Msamaha katika maisha ya familia unatufundisha nini?

38. (a) Kwa nini tunatenda dhambi?
    (b) Dhambi ni nini? (Jibu lina sehemu mbili)
    (c) Tamaa ya kutenda dhambi inatoka wapi?
    (d) Nyoka anasimama badala ya nini katika Biblia baada ya dhambi ya Adamu na Hawa?

Kazi ya ziada.
    (e) Matokeo ya dhambi ni nini?

39. (a) Ni kwa nini Biblia ni ya muhimu kwako? Inakufanya tu kujisikia vizuri kuwa nayo, au ni kitu chenye maana ya kipekee katika maisha yako?
    (b) Ni mara ngapi unaifungua na kuisoma? Kila siku? Kila wiki? Au mara moja-moja tu? Unaisoma yote au baadhi ya vifungu unavyovipenda tu?
    (c) Unaweza kuifungua mahali unapopataka kiurahisi? Unajua Kitabu cha Zaburi kilipo? Yuda kipo wapi? Mika, je?
    (d) Unaweza kuvipata vifungu ndani ya Biblia kuweza kuwaambia watu wengine unayoamini?
    (e) Unaweza kuisema mistari au vifungu kutoka kichwani (bila kusoma), ili kuonesha unachoamini?

Kazi za ziada
    (f) Biblia inakuvutia na kukusisimua kama ni Neno la Mungu?
    (g) Usomaji wako wa Biblia umekusaidia kubadili namna yako ya kufikiri na kuishi katika maisha yako? Kama ndio, kwa namna gani?

40. (a) Neno ‘Eklesia’ lina maana gani?
    (b) Watu wanapaswa kufanya nini ili waweze kuwa na sehemu katika Eklesia ya Mungu?

Kazi ya ziada

(c) Wafuasi wanapaswa waweje wanapokutana kujadili masuala ya Eklesia?

*Kumbuka kuweka jina lako, anwani na namba yako ya kumbukumbu katika karatasi yako ya majibu.*